

Nakutukuza Ee Bwana Kwakuwa umeniokoa

Zaburi 29, 3-4, 5-6ab, 6cd-12-13

Siku ya Mungu Ya kumi na Tatu katika Mwaka B (13e Dim)

$\text{♩} = 75$

Musique : GRACE Mushagalusa Fabrice

S
A

R/Na - ku - tu - ku - za, - ee - Bwa - na, - kwa - ku - wa - u - me - ni - o - ko - a

T
B

9

1/ Ee Bwana, Mungu wangu,
nilikulilia Wewe, ukaniponya;
Ee Bwana, umeondoa roho yangu kuzimuni,
umeniokoa katika wale wanaoshuka shimoni.

2/ Mwimbieni Bwana, enyi waamini wake,
shukuruni jina lake takatifu,
Kwani hasira yake ni ya kitambo kidogo
mapendo yake yadumu maisha yote.

3/ Jioni machozi yanakuja na kukawa,
asubuhi tena kuna shangwe,
Umegeuza kilio changu kuwa mchezo,
umenivulia gunia, ukanivika furaha.